

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Jiji)

**MKOA WA DODOMA**

Tel.: 2354817/2321550

Fax: 2321550



**Ofisi ya Mkurugenziwa Jiji**

S. L. P. 1249

**Dodoma**

Barua pepe: cd@dodomacc.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:  
Kumb. Na. HMD/A 10/2/49

Tarehe: 06 Mei, 2020

Mkurugenzi Mtendaji,  
Kirobe Investment Company Limited,  
S. L. P. 71573,  
DAR ES SALAAM.

**YAH: OMBI LAKO LA KUPATIWA JENGO KWA AJILI YA KUSIMIKA MASHINE  
ZA KUTENGENEZA SOLI ZA VIATU ENEO LA SQ 300.**

Tafadhali rejea barua yako ya tarehe 02/03/2020 yenye kichwa cha habari hapo juu.

Halmashauri ya Jiji la Dodoma inapenda kukutaarifu kuwa imekubali ombi lako la kupanga jengo la Jiji liitwalo ghala la DUDIDECO lililoko karibu na hoteli ya VETA (nyuma ya ofisi za Bunge. Kodi yako ya mwezi itakuwa ni Tshs 3,000,000.00 (milioni tatu tu) kwa mwezi.

Kwa barua hii unatakiwa fufanya malipo kama ifuatavyo:

1. Tshs 15,000.00 gharama za uandaaji wa mikataba, na

2. Tshs 3,000,000.00 kwa ajili ya kodi ya mwezi unaoanza kutumia jengo hilo,

Baada ya kukamilisha malipo hayo, wasilisha nakala ya risiti yenye rangi ya njao ili uweze kuandaliwa mikataba na kukamidhiwa jengo rasmi kwa ajili ya matumizi. Masharti mengine yote yatapatikana kwenye mikataba husika.

Katika ujenzi wa Taifa,

Ellyhuruma M. Mufuruki,  
Kny. Mkurugenzi wa Jiji,  
Jiji la Dodoma

Nakala: Mkurugenzi wa Jiji  
Jiji la Dodoma

aione kwenye jalada

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mkoa wa Dodoma

Anwani ya Simu REGCOM

Simu Nambari:

2324343/2324384

E-Mail No.

ras@dodoma.go.tz

Fax No. 255 026 2320046

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. . BA.122/470/011/38



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
Jengo la Tume ya  
Maendeleo ya ushirika  
Barabara ya Nyerere  
S.L.P. 914,  
**41103 DODOMA.**

03 Machi, 2020

Mkurugenzi wa Jiji,  
Halmashauri ya Jiji,  
Dodoma.

**Yah; MWEKEZAJI WA MASHINE YA KUTENGENEZA SOLI ZA VIATU NA  
VIATU DODOMA.**


Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu,

Mkoa umepokea barua isiyo na Kumb Na.ya tarehe 26 Februari, 2020 kutoka  
Kampuni ya KIROBE yenye mada tajwa hapo juu.

Kampuni ya Kirobe Investment Ltd inajishughulisha na kutoa elimu kwa wachunaji wa ngozi za mifugo kwa lengo la kupata ngozi bora kwa ajili ya kuuza nje ya nchi. Kampuni hii ina stoo nane (8) zinazotunza ngozi kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi katika Wilaya ya Bahi. Mwaka huu Kampuni imeingia makubaliano ya kutengeneza soli na viatu na kampuni iitwayo ENNE BI SRL iliyoko nchini Italy na mwaka kesho itajenga tannary kwa ajili ya kusindika ngozi hadi daraja la mwisho (Finished leather). Ili kufanikisha uwekezaji wake, mwekezaji huyu anahitaji kupata eneo la haraka kwa ajili ya kusimika machine za kusindika ngozi zinazotarajia kuwasili nchini kutoka Italy hivi karibuni.

Kwa barua hii, unaelekezwa kumwezesha mwekezaji huyu kupata jengo ambalo litamwezesha kuanza uzalishaji mara mashine zitakapowasili. Aidha, apatiwe eneo ambalo atajenga kiwanda chake.

Nakutakia utekelezaji mwema.



Aziza R. Mumba

Kny: KATIBU TAWALA WA MKOA  
DODOMA